Unafanya Nini Duniani Kwa Ajili Ya Mbingu?

(What On Earth Are You Doing For Heaven's Sake?)

Na

Ellis P. Forsman

Unafanya Nini Duniani Kwa Ajili Ya Mbingu?

(What On Earth Are You Doing For Heaven's Sake?)

Na

Ellis P. Forsman

Oktoba 17, 2011

Unafanya Nini Duniani Kwa Ajili Ya Mbingu?

Heb. 2:

Somo hili liliwekwa pamoja kwa mara ya kwanza na Howard McCay huko nyuma miaka yaa 1960 baada ya kusikia kiongozi wa chuo akiwahimiza wafungwa kuhusu kazi yake.

Unafanya Nini?

Siyo rafiki au jirani, bali wewe.

Kristo alimwambia Petro amfuate.

Yoh. 21:20-22, "*Petro akageuka akamwona yule mwanafunzi aliyependwa na Yesu anamfuata; ndiye huyo aliyeegama kifuani pake wakati wa kula chakula cha jioni, akasema Bwana ni nani akusalitiye? Basi Petro akamwona huyo akamwambia Yesu, Bwana, na huyu je? Yesu akamwambia, ikiwa nataka huyu akae hata nijapo, imekupasaje wewe? Wewe unifuate mimi.*"

Utimizeni wokovu wenu wenyewe.

Fil. 2:12, "*Basi wapendwa wangu kama vile mlivyotii siku zote, si wakati mimi nilipokuwapo tu, basi sasa zaidi sana mimi nisipokuwapo, utimizeni wokovu wenu wenyewe kwa kuogopa na kutetemeka.*"

Unafanya Nini Kwa Wakati Wako?

Maisha haya ndio wakati pekee tulionao kujiandaa kwa ajili ya mbingu.

- 2 Kor. 6:1-2, "*Nasi tukitenda kazi pamoja naye twawasihi msiipokee neema ya Mungu bure. Kwa maana asema wakati uliokubalikaa nalikusikia; tazama wakati ulikubalika ndio sasa; tazama siku ya wokovu ndiyo sasa.*"
- Heb. 3:12-15, "*Angalieni ndugu zangu usiwe katika mmoja wenu moyo mbovu wa kutokuamini, kwa kujitenga na Mungu aliye hai. Lakini mwonyane kila siku maadamu iitwapo leo; ili mmoja wenu asifanywe mgumu kwa udanganyifu wa dhambi. Kwa maana tumekuwa washirika wa Kristo kama tukishikamana na mwanzo*

wa uthabiti wetu kwa nguvu mpaka mwisho; hapo inenwapo, leo kama mtaisikia sauti yake, msifanye migumu mioyo yenu, kama wakati wa kukasirisha."

Tuna wakati huu uliopo; tuna leo. Jana ilienda. Kesho labda isije.

Kutenda Kunaonyesha Hatua

Wakristo lazima wachangamke katika kumfanyia Kristo kazi.

- Mhu. 12:13-14, "*Hii ndiyo jumla ya maneno yote yamekwisha sikiwa; mche Mungu nawe uzishike amri zake, maana kwa jumla ndiyo impasayo mtu. Kwa maana Mungu ataleta hukumuni kila kazi, pamoja na kila neno la siri, likiwa jema au likiwa baya.*"

- Mat. 25:34-46, "*Kisha mfalme atawaambia wale walioko mkono wake wa kuume, njooni mliobarikiwa na Baba yangu, urithi ufalme mliowekewa tayari tangu kuumbwa ulimwengu. Kwa maana nalikuwa na njaa mkanipa chakula; nalikuwa na kiu mkaninywesha; nalikuwa mgeni mkanikaribisha, nalikuwa uchi mkanivika, nalikuwa mgonjwa mkaja kunitazama; nalikuwa kifungoni mkanijia. Ndipo wenye haki watakapo mjibu, wakisema, Bwana, ni lini tulipokuona una njaa tukakulisha, au una kiu tukakunywesha? Tena ni lini tulipokuona u mgeni, tukakukaribisha, au u uchi tukakuvika? Ni lini tena tulipokuona u mgonjwa au kifungoni, tukakujia? Na mfalme atajibu akiwaambia, amini nawaambia kadiri mlivyomtendea mmojawapo wa hao ndugu zangu walio wadogo mlinitendea mimi. Kisha atawaambia na wale walioko mkono wake wa kushoto, ondokeni kwangu mliolaaniwa mwende katika moto wa milele, aliowekewa tayari ibilisi na malaika zake; kwa maana nalikuwa na njaa msinipe chakula; nalikuwa na kiu msininywesha; nalikuwa mgeni msinikaribishe, nalikuwa uchi msinivike; nalikuwa mgonjwa na kifungoni msije kunitazama. Ndipo hao pia watajibu na kusema, Bwana ni lini tulipokuona wewe una njaa, au una kiu, au u mgeni, au u uchi, au u mgonjwa, au u kifungoni, tusikuhudumie? Naye atawajibu akisema, amini nawambia, kadiri msivyomtendea mmojawapo wa hao walio wadogo hamkunitendea mimi. Na hao watakwenda zao kuingia katika adhabu ya milele; bali wenye haki watakwenda katika uzima wa milele.*"

- Tito 2:14, "*Ambaye alijitoa nafsi yake kwa ajili yetu, ili atukomboe na maasi yote, na kujisafishia watu wawe milki yake mwenyewe, wawe na juhudi katika matendo mema.*"

Zingatia matendo yetu.

Hagai 1:5-7, "*Basi sasa BWANA wa majeshi asema hivi, zitafakarini njia zenu. Mmepanda mbegu nyingi mkavuna kidogo; mnakula lakini hamshibi; mnakunywa lakini hamkujazwa na vinywaji; mnajivika nguo lakini hapana aonaye moto; nay eye apataye mshahara apata mshahara ili kuutia katika mfuko ulitobokatoboka. BWANA wa majeshi asema hivi zitafakarini njia zenu.*"

Lazima tushike amri zake.

- 1 Yoh. 2:3-4, "*Na katika hili twajua ya kuwa tumemjua yeye, ikiwa tunashika amri zake. Yeye asemaye, nimemjua wala hazishiki amri zake, ni mwongo, wala kweli haimo ndani yake.*"
- 2 Thes. 1:7-9, "*Na kuwalipa ninyi mteswao raha pamoja na sisi, wakati wa kufunuliwa kwake Bwana Yesu kutoka mbinguni pamoja na malaika wa uweza wake. Katika mwali wa moto; huku akiwalipiza kisasi wao wasio mjua Mungu, na wao wasioitii injili ya Bwana wetu Yesu; watakaoadhibiwa kwa maangamizi ya milele, kutengwa na uso wa Bwana na utukufu wa nguvu zake.*"

Je tunamtii Mungu na kuzishika sheria zake?

Hakuna aliye sahihi katika mawazo yake ya kidini.

1 Kor. 14:37, "*Mtu akijiona kuwa ni nabii au mtu wa rohoni, na ayatambue hayo ninayowaandikia, ya kwamba ni maagizo ya Bwana.*"

Ni Nini Matokeo Ya Matendo Yetu?

Umilele wetu utategemeana na matendo yetu katika maisha haya.

- Mat. 6:24, "*Hakuna mtu awezaaye kutumikia mabwana wawili; kwa maana atamchukia huyu na kumpenda huyu; ama atashikamana na huyu na kumdharau huyu. Hamwezi kumtumikia Mungu na mali.*"
- Mat. 6:33, "*Bali utafuteni kwanza ufalme wake na haki yake, na hayo yote mtazidishiwa.*"

- 1 Tim. 5:8, "*Lakini mtu yeyote asiyewatunza walio wake, yaaani wale wa nyumbani mwake hasa, ameikana imani, tena ni mbaya kuliko mtu asiyeamini.*"
- Yako. 2:14-20, "*Ndugu zangu yafaa nini mtu akisema ya kwamba anayo imaani, lakini hana matendo? Je ile imani yaweza kumwokoa?ikiwa ndugu mwanaume au ndugu mwanamke yu uchi na kupungukiwa na riziki, na mtu wa kwenu akawaambia, enendeni zenu kwa amani, mkaote moto na kushiba, lakini asiwape mahitaji ya mwili, yafaa nini? Vivyo hivyo na imani isipokuwa ina matendo imekufa nafsini mwake. Lakini mtu atasema, wewe unayo imani, mimi ninayo matendo. Nionyeshe imani yako pasipo matendo, nami nitakuonyesha yangu kwa njia ya matendo. Wewe waamini ya kuwa Mungu ni mmoja, watenda vema. Mashetani nao waamini na kutetemeka. Lakini wataka kujua wewe mwanadamu usiye kitu, kwamba imani pasipo matendo haizai?*"
- Ufu. 20:12, "*Nikawaona wafu wakubwa kwa wadogo, wamesimama mbele ya hicho kiti cha enzi; na vitabu vikafunguliwa, na kitabu kingine kikafunguliwa, ambacho ni cha uzima; na hao wafu wakahukumiwa katika mambo hayo yaliyoandikwa katika vile vitabu, sawasawa na matendo yao.*"

Hatutaweza kufika mbinguni kama hatufanyi chochote.

- 2 Pet. 3:9, "*Bwana hakawii kuitimiza ahadi yake , kama wengine wanavyokudhani kukawia, bali huvumilia kwenu, maana hapendi mtu yeyote apotee, bali wote wafikilie toba.*"
- Mat. 7:21, "*Si kila tu aniambiaye Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni; bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni.*"
- Luka 10:2, "*Akawambia mavuno ni mengi, lakini watenda kazi ni wachache; basi mwombeni Bwana wa mavuno apeleke watenda kazi katika mavuno yake.*"
- 2 Tim. 4:2, "*Lihubiri neno uwe tayari wakati ukufaao na wakati usiokufaa, karipia, kemea, na kuonya kwa uvumilivu wote na mafundisho.*"

Jinsi Ya Kufanyika Mkristo

Tii kutoka moyoni.

Rum. 6:17, "*Lakini Mungu na ashukuriwe kwa maana mlikuwa watumwa wa dhambi, lakini mliitii kwa mioyo yenu ile namna ya elimu ambayo mliwekwa chini yake.*"

Amini.

Heb. 11:6, "*Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa dhawabu wale wamtafutao.*"

Tubu.

- Mdo. 2:38, "*Petro akwaambia tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*"
- Luka 13:3, "*Nawaambia sivyo; lakini msipotubu ninyi nyote mtaangamiaa vivyo hivyo.*"

Kiri.

- Rom. 10:9, "*Kwa sababu ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu utaokoka.*"
- Mat. 10:32, "*Basi kila mtu atakayenikiri mbele ya watu, nami nitamkiri mbele za Baba yangu aliye mbinguni.*"

Ubatizwe.

- Gal. 3:27, "*Maana ninyi nyote mliobatizwa katika Kristo mmemvaa Kristo.*"
- Mdo. 2:38, "*Petro akwaambia tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*"

Dini nyingi zinaacha ubatizo kama kitu mhimu kwa ajili ya wokovu. Dini zingine zinawabatiza watoto wachanga, lakini mtoto mchanga anawezaje kuamini, kutubu, na kumkiri Kristo? Kunyunyiza – ubatizo? Unaweza kuita bata mbwa, lakini hiyo haiwezi kumfanya awe mbwa. Kanisa la Kibaptist wakati mwingine wanabatiza, lakini haifanywi kwa ajili ya ondoleo la dhambi.

1 Pet. 3:21, "*Mfano wa mambo hayo ni ubatizo, unaowaokoa ninyi pia siku hizi; siyo kuweka mbali uchafu wa mwili, bali jibu la dhamiri safi mbele za Mungu, kwa kufufuka kwake Yesu Kristo.*"

Hitimisho

Unafanya nini katika dunia kwa ajili ya mbingu?